**CHUO CHA MAFUNZO YA UFUNDI STADI NA HUDUMA – VETA ULYANKULU**
**MAHITAJI YA MUHIMU YA KUJIUNGA NA CHUO KWA MWAKA 2025**

**CHUO KITAFUNGUA TAREHE 13/01/2025**

**KUCHAGULIWA KUJIUNGA NA CHUO CHA MAFUNZO YA UFUNDI STADI**

**VETA NGORONGORO– 2025 (LEVEL I)**

## 1. UTANGULIZI

Uongozi wa Chuo cha Ufundi Stadi VETA NGORONGORO, unakupongeza na kukufahamisha kuwa umechaguliwa kujiunga na Chuo cha ufundi stadi VETA NGORONGORO, katika fani tajwa Mwanzoni mwa fomu. Nafasi hii ni adimu sana, hata hivyo wewe umekuwa miongoni mwa vijana wachache waliobahatika kupata nafasi miongoni mwa wengi walioomba. Ni matumaini yetu kuwa utaitumia vema nafasi hii, katika kipindi chako cha mafunzo ili uweze kujijengea maarifa, stadi na mwelekeo wa kutosha kukidhi mahitaji ya kuwa fundi stadi wa sasa na baadae.

Mafunzo ya ufundi stadi yameandaliwa kwa lengo la kuwajengea umahiri kitaaluma, na katika stadi za kazi katika misingi ya kwenda kuajiriwa au kujiajiri baada ya kuhitimu.

## 2. MAHALI CHUO KILIPO NA JINSI YA KUFIKA CHUONI

Mahali chuo kilipo

Chuo cha ufundi stadi VETA NGORONGORO, kipo Mkoani Arusha, Wilaya ya Ngorongoro, Tarafa ya Sale, Kata ya Samunge, Kijiji cha Samunge. Chuo kipo umbali wa Km 384 kutoka Arusha.Kutoka Arusha unapanda gari ziendazo Loliondo unashuka Mditto (katikati ya safari).

**MAELEKEZO MUHIMU.**

1. Unatakiwa kununua vifaa vifuatavyo kwa matumizi yako chuoni:
   - 1.1 Mashati mawili meupe (mikono mifupi) ya Tetron.
   - 1.2 Jozi moja ya viatu nyeusi vya ngozi, visigino vifupi vya Kamba
   - 1.3 Vifaa vya hesabu (mathematical set).
   - 1.4 Daftari 7 kubwa.
   - 1.5 Karatasi nyeupe A4 (Vista Plus) au (Nopa) rimu moja kwa ajili ya mitihani.
   - 1.6 Sweta rangi ya blue.
   - 1.7 Fyekeo moja (1)
   - 1.8 Jembe lenye mpini moja (1)

2. Unatakiwa kilipia kiasi cha fedha kama ilivyofafanuliwa nyuma ya maelezo haya.

3. Fedha ikishalipwa hairudishwi, fedha za tahadhari (caution money) ikiwa hazikutumika zitarudishwa.

6. Unatakiwa kufuata sheria na taratibu zote za Chuo zilizoambatanishwa kwenye barua hii.

7. Wanafunzi wakifika mwaka wapili, watakwenda kwenye mafunzo viwandani (Field/Industrial Training), kwa muda wa miezi miwili-mitatu kutegemea fani yake hivyo, Mzazi atawajibika kugharimia gharama za chakula na mahitaji mengine ili kumuwezesha kijana kupata mafunzo kwa vitendo bila usumbufu.

**CHUO KITAFUNGUA TAREHE 13/01/2025**

VOCATIONAL EDUCATION AND TRAINING AUTHORITY

The Medical Officer                                        Date: …..../..…./………..

………………………………………………

………………………………………………

……………………………………………….

……………………………………………….

REQUEST FOR MEDICAL EXAMINATION:

Name of Trainee
………………………………………………………………………………………………..

Please examine the above-named trainee to his/her fitness to undergo training and subsequently work as a/an ………………………………………………………………………………….

i) Eyesight ……………………………………………………….

ii) Hearing ……………………………………………………….

iii) Asthma ……………………………………………………….

iv) Other-serious diseases ……………………………………………………….

v) Pregnancy test ……………………………………………………….

Medical certificate:

I have examined the above named and consider that he/she is physically fit/unfit for training as above.

Designation: …………………………… Signature & Official Stamp: ………………………………………

Date: ………………………………………

**CHUO KITAFUNGUA TAREHE 13/01/2025**

MAMLAKA YA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI STADI (VETA)

FOMU YA KUKUBALI NAFASI YA MAFUNZO YA UFUNDI STADI

(a) MWANACHUO

Mimi …………………………………………………………..………………… ninakubali nafasi ya mafunzo katika fani niliyopangiwa, pamoja na kuzingatia sheria na kanuni za chuo ambazo nimezisoma na kuzielewa vizuri.

Sahihi: …………………………………… Tarehe: …………………………………

(b) MDHAMINI

Mimi ………………………………………………………………………………………………………….
Ninathibitisha kuwa ninamdhamini aliyetajwa hapo juu na nitamlipia gharama zote za mafunzo (ada) na michango mingine. Pamoja na nauli wakati wa kwenda Chuoni na kurudi nyumbani kwa likizo na baada ya mafunzo kama ilivyoelekezwa katika maelezo ya kujiunga na chuo wakati wote wa mafunzo.

Sahihi: ………………………………..…………………………… Tarehe: ………………………

**CHUO KITAFUNGUA TAREHE 13/01/2025**

## MAMLAKA YA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI STADI (VETA)
## SHERIA ZA CHUO KWA WANAFUNZI WA KUTWA

Ili kufanikisha mafunzo ya awali ya Ufundi kila mwanafunzi anatakiwa kufuata Sheria zifuatazo:-

**1.** MAHUDHURIO

(a) Kila mwanafunzi anatakiwa kufika Chuoni kabla ya saa 1.30 asubuhi. Atakaechelewa hataruhusiwa kuingia Chuoni.

(b) Mwanafunzi hatakiwi kutoka nje ya Chuo kwenda nyumbani, hospitali au sehemu nyingine yoyote ile bila ya kuruhusiwa na mwalimu (Mkuu wa fani husika)

(c) Mwanafunzi apatapo matatizo ya msiba, kuuguliwa au kuugua mwenyewe ni lazima habari hizo/taarifa zifike Chuoni, bila ya kufanya hivyo kutamuingiza mwanafunzi kwenye makosa mengine kama utoro.

(d) Mahudhurio chini ya 85% mwanafunzi hataruhusiwa kufanya mitihani.

(e) Karakana/madarasa na vifaa vitumiwe kufuatana na shughuli zake. Hairuhusiwi kuchora au kuandika kwenye kuta za majengo ya Chuo.

**2.** MAVAZI

(a) Sare ya Chuo ni suruali ya bluu na shati Jeupe mikono mifupi. Sare hiyo ivaliwe wakati wote mwanafunzi awapo Chuoni na wakati wa safari ya kuja Chuoni na kurudi nyumbani. Wakati wote shati liwe limechomekewa. Ni marufuku kuvaa nguo za kubana.

(b) Ovaroli livaliwe wakati wa vipindi vya kazi za mikono tu.

(c) Viatu vyenye visigino virefu na kandambili au sandosi (sandals) haviruhusiwi kuvaliwa Chuoni wakati wa masomo.

**3.** USAFI WA MWILI

(a) Hairuhusiwi kuvaa hereni, pete, bangili, mkufu na mapambo ya aina yoyote ile kwa kipindi chote cha mafunzo.

(b) Hairuhusiwi kutumia vipodozi au manukato yanayotoa harufu kali.

(a) Nywele kwa wavulana
- (i) Zikatwe ziwe fupi sana, KIPARA, KIDUKU, PANKI hairuhusiwi kabisa.
- (ii) Ndevu, na Mustachi haviruhusiwi

(b) Nywele kwa wasichana
- (i) Zikatwe ziwe fupi au zisukwe kwa mistari mitano au sita ya kurudi nyuma (twende kilioni).

(e) Huruhusiwi kufuga Kucha kwa namna yeyote wala kupaka rangi.

**4.** WIZI WA MALI ZA CHUO AU MALI YA MTU YEYOTE YULE:

(a) Vitendo vyovyote vya wizi haviruhusiwi. Pindi ikibainika mwanafunzi ameiba mali ya Chuo au ya mwanafunzi mwenzake, hatua za kisheria zitachukuliwa mara moja ikiwa ni pamoja na kufukuzwa Chuo.

(b) Ukipoteza vifaa vya Chuo utatakiwa kulipa gharama kamili ya kifaa na ukakinunue kifaa chenyewe.

(c) Hairuhusiwi mwanafunzi kuingia na kifaa chochote kile kinachofanana na vile vilivyoko ndani ya Chuo.

(d) Mwanafunzi atapekuliwa wakati wa kutoka karakana na getini.

**5.** UGOMVI:

Ugomvi, kupigana na kushambuliana ni makosa ya jinai. Atakayepatikana akijihusisha na matendo ya namna hiyo hatua za kisheria zitachukuliwa mara moja.

**6.** ULEVI:

Iwapo itabainika mwanafunzi amelewa, au kuonekana katika sehemu za kileo, anavuta bangi au madawa ya kulevya hatua za kisheria zitachukuliwa mara moja.

**7.** MAPENZI:

(a) Uhusiano wa kimapenzi Chuoni kati ya mwanafunzi na mwanafunzi au kati ya mfanyakazi na mwanafunzi hairuhusiwi kabisa.

(b) Mwanafunzi wa kiume au wa kike haruhusiwi kuingia maeneo wanayoishi wafanyakazi wa Chuo bila kibali au ruhusa.

**8.** MIGOMO:

Migomo ni marufuku, na kuchochea migomo ni kosa lisilostahimilika. Atakayeshawishi au kusababisha migomo hatua za kisheria zitachukuliwa mara moja.

**9.** LUGHA:

Lugha inayotumika kuendeshea masomo ni Kiingereza/Kiswahili hivyo ni wajibu wa kila mwanafunzi kujifunza hizo lugha.

**10.** Jina lisibadilishwe mpaka ziwepo sababu na hati maalum kwa uthibitisho na ajulishwe Mkuu wa Chuo mara moja.

**11.** Ni marufuku kwa mwanachuo kuja na simu za mkononi Ikigundulika una simu au simu ikiita wakati wa vipindi utanyang’anywa na itahifadhiwa mpaka utakapomaliza Chuo.

**CHUO KITAFUNGUA TAREHE 13/01/2025**

## ONGEZEKO LA SHERIA KWA MWANACHUO WA BWENI

12. Mwanachuo yeyote anayeruhusiwa kutoka nje ya eneo la Chuo wakati wa saa za masomo anapaswa kuwa na kitambulisho cha Chuo, sare ya Chuo na atajiandikisha lango kuu. Mwanafunzi atakayeonekana nje ya maeneo ya Chuo bila kuwa na sare atachukuliwa hatua kali za kinidhamu ikiwa ni pamoja na kufukuzwa Chuoni.

13. Haitaruhusiwa kupikia chakula bwenini, na atakayekiuka sheria hii atachukuliwa hatua kali.

14. Ruhusa ya kutoka Chuoni ni lazima iizinishwe na mwalimu wa fani husika.

**CHUO KITAFUNGUA TAREHE 13/01/2025**

## MCHANGANUO WA MAHITAJI WA MWANAFUNZI KWA MWAKA 2025

| S/N | Aina ya malipo | MUHULA WA I-2025 | | MUHULA WA II- 2025 | |
|---|---|---|---|---|---|
| | | BWENI | KUTWA | BWENI | KUTWA |
| 1 | Ada ya Mafunzo | 120,000 | 60,000 | 00 | 00 |
| 2 | Fedha za Uniform (suruali 2) | 40,000 | 40,000 | 00 | 00 |
| 3 | Overcoat/overoll moja | 30,000 | 30,000 | 00 | 00 |
| 4 | Ada ya Mtihani (CBA) | 00 | 00 | 25,000 | 25,000 |
| 5 | Tshirt | 15,000 | 15,000 | 00 | 00 |
| 6 | Fedha ya Ukarabati (Hairudishwi) | 20,000 | 20,000 | 00 | 00 |
| 7 | Godoro pamoja na Neti | 20,000 | 00 | 00 | 00 |
| 8 | Michezo | 10,000 | 10,000 | 00 | 00 |
| 9 | Nembo ya VETA | 5,000 | 5,000 | 00 | 00 |
| 10 | Kitambulisho | 5,000 | 5,000 | 00 | 00 |
| 11 | Kuchangia sherehe ya mahafali | 00 | 00 | 25,000 | 25,000 |
| | JUMLA | 265,000 | 185,000 | 50,000 | 50,000 |
| | MAHITAJI MENGINE UNAYOTAKIWA KUJA NAYO | | | | |
| 12 | Mashati mwawili (2) meupe ya tetron ya mikono mifupi | Uje nayo | Uje nayo | | |
| 13 | Viatu vya Ngozi jozi moja (1) nyeusi | Uje navyo | Uje navyo | | |
| 14 | Nguo na Viatu vya Michezo (bluu) | Uje nazo | Uje nazo | | |
| 15 | Mathematical set, 1 | Uje nayo | Uje nayo | | |
| 16 | Scientific calculator, 1 | Uje nayo | Uje nayo | | |
| 17 | Vyombo vya kuogea, kufulia na kulia chakula | Uje navyo | - | | |
| 18 | Madaftari 07 makubwa, Quire 3 | Uje nayo | Uje nayo | | |
| 19 | Ream ya karatasi (A4) 1 | Uje nayo | Uje nayo | | |
| 20 | Spring file 1 | Uje nalo | Uje nalo | | |
| 21 | Sweta la rangi ya Dark bluu | Uje nalo | Uje nalo | | |

**CHUO KITAFUNGUA TAREHE 13/01/2025**

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| 22 | Shuka 2 za bluu. | Uje nazo | - | | |
| 23 | Safety boot, Jozi moja (nyeusi) | Uje nayo | Uje nayo | | |
| 24 | Jembe lenye mpini 1 | Uje nalo | Uje nalo | | |
| 25 | Fyekeo 1 | Uje nalo | Uje nalo | | |
| 26 | Kitambulisho au namba ya NIDA | Uje nayo | Uje nayo | | |